*BUSEGA DC JARIDA*
**Toleo Na. 3**
**OKTOBA, 2021**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA




TOLEO LA ROBO YA KWANZA 2021/2022



**Linatolewa Na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Busega, S.L.P 157**

www.busegadc.go.tz

@busegadc busegadc

@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

YALIYOMO

**UTANGULIZI** .................................................. 1

**Lengo la Jarida**.............................................. 1

**Habari na Matukio Yaliyojiri Robo ya Kwanza 2021/2022**…………………………………………………2-28

## UTANGULIZI

*Halmashauri ya Wilaya ya Busega ni mojawapo ya Halmashauri 6 zilizopo Mkoa wa Simiyu. Halmashauri ya Wilaya ya Busega imeanzishwa mwaka 2013 ikiwa ina Tarafa 2, Kata 15, Vijiji 59 na Vitongoji 362. Halmashauri ya Wilaya ya Busega ina jumla ya Madiwani 20 ambapo madiwani 15 ni wa kuchaguliwa na Madiwani 5 ni wa viti maalum.*

*Kijiografia wilaya ya Busega inapakana na Wilaya ya Magu upande wa Magharibi, Wilaya ya Ukerewe upande wa kaskazini, Wilaya ya Bunda upande wa mashariki na kwa upande wa kusini imepakana na Wilaya ya Bariadi na Itilima. Wilaya ya Busega ina jumla ya ukubwa wa Kilometa za mraba 2129, ambapo Kilometa za mraba 1524 ni nchi kavu, na Kilometa za mraba 605 ni sehemu ya maji (Ziwa Viktoria).*

## LENGO LA JARIDA

Busega DC Jarida linalenga kuhabarisha na kuelezea shughuli za matukio mbalimbali ya Kiserikali Wilayani Busega, shughuli za utekelezaji wa Miradi na Matukio mengine muhimu Wilayani Busega. Pia Jarida hili linalenga kupanua wigo wa wakazi wa Busega na walio nje ya Busega kupata Habari na taarifa mbalimbali za shughuli za maendeleo zinazotekelezwa Wilayani humo. Jarida hili huandaliwa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Busega. Toleo la Jarida hili huchapishwa kila baada ya Miezi Mitatu. Pia kupata taarifa, matangazo na miongozo mbalimbali unaweza kutembelea Tovuti ya Halmashauri: www.busegadc.go.tz na Mitandao ya Kijamii Instagram: Busega_Dc; Facebook: Halmashauri ya Wilaya ya Busega na YouTube Channel: BusegaDc

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

# DED Sayore Akibidhiwa Ofisi



Picha: Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bw. Anderson Kabuko (aliyesimama kulia) akimkabidhi nyaraka mbalimbali Mkurugenzi Mteule Bi. Veronica Sayore (aliyesimama kushoto)

Makabidhiano ya Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega yamefanyika siku ya tarehe 09 Agosti 2021. Bi. Veronica Sayore ambae ni Mkurugenzi mteule wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega amekabidhiwa Ofisi na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bw. Anderson Kabuko.

Katika makabidhianao hayo Bi. Sayore amesema anategemea ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi wa Wilaya pamoja na Watumishi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega na kusisitiza kwamba bila ushirikiano hakuna kitakachoweza kufanyika. Aidha Bi. Sayore ametoa pongezi kwa

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bw. Anderson Kabuko kwa kipindi chote alichoweza kuhudumu kama Mkurugenzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Busega na kwa hatua kubwa ya utendaji wake.

Kwa upande wake, aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bw. Anderson Kabuko amewashukuru Watumishi wote na kuahidi kwamba ataendelea kutoa ushirkiano pale watakapoona inafaa ili kuendelea kuleta maendeleo kwa wananchi wa Busega. Mwenyeketi wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Mhe. Sundi Muniwe amesema anaamini watafanya kazi kwa ushrikiano na anamkaribisha sana Bi. Sayore katika Halmashauri ya Wilaya ya Busega.

Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria ametoa shukrani kwa Bw. Anderson Kabuko kwa kipindi walichoweza kufanya kazi pamoja na anaamini kwamba Mkurugenzi aliyekabidhiwa Ofisi ataendeleza ushirikiano wa utendaji kazi kati ya Ofisi ya Mkurugenzi na Ofisi yake. Makabidhiano hayo yamehudhuriwa na Kamati ya Ulizni na Usalama Wilaya ya Busega, baadhi ya Madiwani, Wakuu wa Idara na Vitengo na baadhi ya Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega.

## Baraza la Madiwani Wataka Usimamizi Bora wa Fedha za Miradi ya Maendeleo Zitokanazo na Mapato ya Ndani

Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Busega wametaka kuwepo kwa usimamizi bora wa Fedha za Miardi ya Maendeleo zinazotokana na Mapato ya Ndani. Madiwani hao wameyasema hayo wakati wa kikao cha Baraza la kufunga Mwaka kwaajili ya kupokea Taarifa ya Utendaji na Uwajibikaji wa Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 lililofanyika tarehe 27 Agosti 2021.

Awali, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Mhe. Sundi Muniwe amesema ni vyema kuhakikisha fedha zinazoletwa na Serikali na zile

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

zinazotokana na mapato ya ndani zinatumika kwa wakati ili kutekeleza miradi mbalimbali katika wakati uliopangwa. Aidha, Mhe. Muniwe amesema kwamba usimamizi bora wa fedha za miradi unaenda sambamba na uchapaji kazi kwa Watumishi.

Wajumbe wa Baraza hilo wamesema kwamba wanatamani kuendelea kuona



**Pichani ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Mhe. Sundi Muniwe (wa pili kutoka kulia), Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe. Ng'habi Mojo (wa tatu kutoka kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bi. Veronica Sayore (wa kwanza kulia) na Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria.**

Miradi ya Maendeleo inakamilika kwa wakati ili kupunguza adha ya Wananchi ya kupata huduma. Aidha, Madiwani wamesema kwamba iwapo Asilimia 40 ya makusanyo ya ndani itasimamiwa na kupelekwa kwa wakati katika Miradi ikiwemo ya Ujenzi wa Madarasa na Zahanati itasaidia kuondoa changamoto kwa wananchi katika baadhi ya maeneo yenye changamoto kubwa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bi. Veronica Sayore amesema katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022, tayari bajeti imetengwa kumalizia Miradi ya Maendeleo iliyoanza kutekelezwa. Bi. Sayore ameongeza kwamba tayari kuna juhudi za kuongeza makusanyo ya ndani ili kupata fedha za kutosha zitakazopelekwa kutumika kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Pamoja na hayo, Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega wameweza kuipokea taarifa hiyo ya

Utendaji na Uwajibikaji wa Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Pamoja na hayo, mengineyo yaliyoibuka wakati wa kikao cha Baraza hilo ni pamoja na asiimia 10 ya mikopo inayotolewa na Halmashauri kwa makundi ya Wanawake, Vijana na Walemavu, huku Madiwani wakihoji juu ya uchelewaji wa urejeshwaji wa fedha kutoka kwa wanaofadikia na Mikopo hiyo.

Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Busega, Bw. Dismas Ijagala amesema kuna ongezeko kubwa la urejeshwaji wa fedha zilizokopeshwa ukilinganisha na hapo awali na hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa kwa wote ambao hawarejeshi fedha hizo kwa wakati ikiwemo kuwafikisha katika mamlaka husika ikiwemo Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao. Baraza hilo la kufunga mwaka limefanyika ikiwa ni ishara ya kuanza Mwaka mpya wa Fedha 2021/2022.

## Ukusanyaji Mapato ya Ndani Kipaumbele cha Kimkakati



Picha: Diwani wa Kata ya Nyashimo Mhe. Mickness Mahela (aliyekaa kulia) na Diwani wa Kata ya Lutubiga Mhe. Agnes Mayuma (aliyekaa kushoto) wakifuatilia kwa umakini kikao cha Baraza la Madiwani.

Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Busega wamesema suala la ukusanyaji wa mapato ni kipaumbele cha kimkakati ikiwa ni sehemu ya kuongeza tija katika ukusanyaji mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani. Hayo yamesemwa na Madiwani wakati wa Baraza la Madiwani robo ya Nne lililofanyika siku ya tarehe 20 Agosti 2021 katika ukumbi wa Silisos.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Mhe. Sundi Muniwe amesema ni muhimu kusimamia na kutilia mkazo wa makusanyo ya ndani ili kuongeza makusanyo ya mapato ya Halmashauri. Mhe. Muniwe amesema

www.busegadc.go.tz
@busegadc
@busegadistrict
busegadc
halmashauri ya wilaya ya busega

Halmashauri haina budi kutatua changamoto za ukusanyaji mapato ili kazi ya ukusanyaji ifanyike kwa ufanisi mkubwa. "Tuhakikishe tunaandaa mazingira rafiki ikiwemo kuwalipa wote wanaohusika na ukusanyaji wa mapato kwa wakati ili kuzuia mianya ya wizi wa fedha", aliongeza Mhe. Muniwe.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria amesema ni vyema kuhakikisha mapato yanaongezeka huku amewaomba waheshimiwa Madiwani kuwa na misimamo kuhusu suala la ukusanyaji wa mapato kwani wana nafasi kubwa sana katika kuijenga Wilaya. Mhe. Zakaria amesema Halmashauri ya Wilaya ya Busega inaweza kukusanya mapato zaidi ya hapo awali.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bi. Veronica Sayore amesema suala la ushirikiano ni muhimu katika kutekeleza majukumu aliyonayo ikiwemo suala la ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo vya ndani. "Hiki ni kikao changu cha kwanza cha Baraza, naamini nitapata ushirikiano kutoka kwenu, ili tuendeshe Halmashauri kwa pamoja na kusimamia majukumu yote", aliongeza Bi. Sayore.

Aidha, Madiwani wamepongeza hatua mbalimbali zinazofanywa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega katika suala la ukusanyaji wa mapato, na kuahidi kwamba watashirikiana na Mkurugenzi Mtendaji kuimarisha mapato ya Halmashauri. Pamoja na hayo baraza hilo, limeweza kuazimia masuala mengine ikiwemo kufutwa kwa suala la mwekezaji aliyetaka kununua ekari 100 katika Viwanja vya Nyanza vinavyomilikiwa na Halmashauri kwa kile kinachoelezwa kutokuwa na uhakika na mwekezaji huyo.

## Wazazi Waaswa Kushiriki Vyema katika Shughuli za Sekta ya Elimu



**Picha: Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria akiongea na wanafunzi wa Darasa la Saba wakati wa maandalizi ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi Uliofanyika tarehe 8 hadi 9 Septemba 2021.**

www.busegadc.go.tz
@busegadc
@busegadistrict
busegadc
halmashauri ya wilaya ya busega

Wazazi Wilayani Busega wameaswa kushiriki vyema katika masuala ya Elimu ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi wanaohitimu elimu ya Msingi. Hayo yamesemwa na Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria alipokutana na wanafunzi wa Darasa la Saba wawakati wa maandalizi ya kufanya mtihani wa kuhitimu shule ya Msingi. Katika ziara ya kukutana na wanafunzi hao Mhe. Zakaria amesema hakuna budi wazazi kusimama mstari wa mbele katika kuhakikisha Watoto wanapata haki ya Elimu.



**Picha: Wanafunzi wa Darasa la Saba Waliofanya mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi mwaka 2021 kwa makini wakisikia maelezo kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria, mtihani uliofanyika tarehe 8 hadi 9 Septemba 2021.**

Aidha, Mhe. Zakaria amesema hatowavumilia wazazi ambao watakuwa sababu ya kukatisha masomo wanafunzi kwasababu mbalimbali ikiwemo kuwaozesha au kuwashughulisha kazi mbalimbali ambazo zitawafanya waaache shule.

Afisa Elimu Wilaya ya Busega Shule za Msingi Bw. Gidion Bunto amesema ni wakati umefika kwa wazazi kushirikiana na walimu ili kutokomeza suala la utoro kwani wapo wanafunzi wengi ambao hutoka nyumbani Kwenda shule lakini huwa hawafiki shuleni. Bw. Bunto amesema wazazi

wengi hawajui kama watoto wao hawahudhurii vipindi mashuleni hivyo ni vyema wazazi washirikiane na walimu ili kujua maendeleo ya watoto wao.

Wanafunzi wapatao 7,539 wilayani Busega wanasajiliwa kwaajili ya kufanya mtihani wa kuhitimu elimu ya Msingi ambapo kati yao, wavulana ni 3,598 na wasichana ni 3,941 ukilinganisha na mwaka jana ambapo waliofanya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi ni wanafunzi 6,562 ambapo wavulana ni 3,158 na wasichana ni 3,404. Mtihani wa kumaliza elimu ya Msingi umefanyika tarehe 8 na 9 Septemba 2021.

# Makampuni Yanayonunua Pamba Wilayani Busega Kulipa Madeni ya Kodi



**Picha: Mwakilishi wa Kampuni mojawapo ya Kununua Pamba Wilayani Busega akitoa hoja wakati wa kikao na Viongozi wa Wilaya ya Busega.**

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

***Inatoka Ukurasa wa 8***

**M**kuu wa wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria ameyataka makampuni yanayonunua Pamba Wilayani Busega kuhakikisha wanalipa madeni ya tozo na kodi za Serikali ifikapo tarehe 10 Oktoba 2021. Zakaria ameyasema hayo wakati wa kikao na wadau wa Pamba Wilayani Busega kilichofanyika tarehe 16/09/2021 katika ukumbi wa Shule ya Msingi Nyashimo.

“Kampuni zote zenye madeni ya kodi zilipe madeni yao ifikapo tarehe 10 Oktoba 2021, kwani miongoni mwa kampuni hizo zimekuwa zikisumbua sana katika ulipaji kodi ambao unakusanywa na Halmashauri”, aliongeza Zakaria.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bi. Veronica Sayore ameyataka makampuni yenye madeni kufika Ofisini kwake kuhakiki madeni hayo kwaajili ya kulipa.

Aidha, Katika kikao hicho suala la kuongeza tija ya Uzalishaji wa zao la pamba lilichukua nafasi, pamoja na mengineyo suala la kuhakikisha mbolea inafika kwa wakati kwa wakulima lilijadiliwa, huku wadau wa pamba wakitaka uwepo wa ushirikiano baina ya mkulima, vyama vya Msingi vya ushirika (AMCOS) na makampuni yanayonunua Pamba.

Afisa kilimo Wilaya ya Busega Bw. Juma Chacha amezitaka kampuni zinazonunua Pamba Wilayani Busega kushirikiana kwa ukaribu na wakulima hasa kwenye suala la upelekaji wa mbolea mashambani kwani wakulima wengi wameshindwa kufikisha mbolea mashambani kutokana na kutokuwa na uwezo wa kufanya hivyo.

Kikao hicho kimefanyika ikiwa ni Utekelezaji wa mikakati ya kuongeza tija ya zao la Pamba Wilaya ya Busega kwa kuzalisha tani 50,000, huku Mkoa ukiweka lengo la kuzalisha tani 500,000. Mikakati hiyo iliwekwa tarehe 22/08/2021 Wilayani Meatu wakati wa majumuisho ya kampeni ya kuongeza tija ya zao la Pamba iliyofanyika Mkoa wa Simiyu.

www.busegadc.go.tz
@busegadc
@busegadistrict
busegadc
halmashauri ya wilaya ya busega

# DED Sayore Aweka Mikakati Kudhibiti Mianya ya Upotevu wa Mapato ya Vyanzo vya Ndani

Katika hatua ya kuhakikisha kwamba mapato ya Halmashauri yanaongezeka, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bi. Veronica Sayore ameongoza timu ya Watumishi kukusanya mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani Bi. Sayore ameiongoza timu hiyo kukusanya mapato yatokanayo na shughuli za uvuvi katika Mwalo wa Nyamikoma uliopo Kata ya Kabita.

Bi. Sayore amesema kwamba ukusanyaji wa mapato ni suala la kila Mtumishi kwani kwa kuweka mlengo wa kushirikiana kwa pamoja katika ukusanyaji wa mapato kutasaidia ongezeko la mapato ya Halmashauri. Aidha, Bi Sayore amesisitiza kwamba suala la mapato ni Msingi wa Maendeleo ya Wilaya, hivyo hakuna budi kulisimamia kwa dhati.

Bi. Sayore amesema Halmashauri imeweka mikakati madhubuti ili kuhakikisha ushuru unakusanywa, lakini ili kukusanya kwa tija ni lazima kuzuia mianya ya utoroshwaji wa bidhaa zitokanazo na uvuvi na vyanzo vinginevyo. Aidha, Bi. Sayore amesema ukusanyaji wa mapato



Picha: Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bi. Veronica Sayore (wa kwanza kulia) akiwa na Watumishi wa Halmashauri katika zoezi la Ukusanyaji mapato katika Mwalo wa Buyolwa.

www.busegadc.go.tz
@busegadc
@busegadistrict
busegadc
halmashauri ya wilaya ya busega

ni suala endelevu hivyo ataendelea kuhakikisha anasimamia vyema ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vingine.

Wavuvi na Wafanyabiashara wanakiri kwamba upatikanaji wa mazao ya uvuvi ni mdogo kwa sasa ukilinganisha na miaka ya nyuma, hali ambayo imesababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa. Kwa upande mwingine Wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi wanakiri kwamba wapo miongoni mwa wafanyabiashara ambao sio waaminifu katika suala la ulipiaji ushuru lakini walio wengi hulipia ushuru bila shida.

Mapato yanayotokana na shughuli za uvuvi yanachangia kwa zaidi ya asilimia 13 katika bajeti ya makusanyo ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya

amesema hatowaonea aibu wote ambao watagundulika kutotumia mfumo

## Watumishi Kada ya Afya Busega Wapata Mafunzo ya Mfumo wa GoT-HoMIS; Watakaokaidi Kutumia hatua Kali Kuchukuliwa Dhidi Yao

Watumishi kada ya Afya Wilayani Busega wamepewa Mafunzo ya Mfumo wa Kuhifadhi Taarifa na ukusanyaji Mapato ijulikanao kama GoT-HoMIS ambao hutumika kwa Ngazi ya Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati. Mafunzo hayo yamefanyika kwa siku mbili tarehe 29 hadi 30 Julai 2021 katika ukumbi mdodgo wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega.

Akifunga Mafunzo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria

wa GoT-HoMIS, na hatua kali zitachukuliwa dhidi yao.

Nae aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega, Bw. Anderson Kabuko amesema Vituo vya Afya na Zahanati ambazo hazitumii mfumo wa GoT-HoMIS kumekuwa na makusanyo madogo ukilinganisha na Vituo vya Afya na Zahanati ambazo mfumo unatumika. Bw. Kabuko amesema baada ya Mafunzo hayo atafutilia kwa uaribu matumizi ya mfumo



**Picha: Watumishi wa Afya wakipata mafunzo mfumo wa GoT-Homis, mafunzo yaliyofanyika katika ukumbi wa Ofisi za Halmashauri.**

huo katika maeneo yote ya kutolea huduma za Afya.

Kwa upande mwingine, Mhe. Gabriel Zakaraia ametoa tahadhari kwa wote ambao wanajihusisha na wizi wa dawa katika maeneo ya kutolea huduma za Afya na kusisitiza kwamba, yeyote atakebainika kuiba dawa atachukuliwa hatua ili iwe fundisho kwa wengine.

www.busegadc.go.tz
@busegadc
busegadc
@busegadistrict
halmashauri ya wilaya ya busega

# Kamati ya Elimu, Afya na Maji Yataka Uboreshwaji wa Miundombinu Mashuleni



Picha: Kamati ya Elimu, Afya na Maji ikiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Vumi Magoti ikiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo.

Kamati ya Elimu, Afya na Maji ya Halmashauri ya Wilaya ya Busega imetaka kuboreshwa kwa miundombinu katika mashule ili kutengeneza mazingira rafiki zaidi kwa Walimu na Wanafunzi. Kamati hiyo ambayo imefanya ziara ya siku moja katika Shule za Msingi za Ilumya na Mwabuduli kwa lengo la kukagua miundombinu siku ya tarehe 03 Agosti 2021.

Akiongoza ziara hiyo Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Vumi Magoti amesema kuna uhusiano mkubwa wa mazingira ya Shule na elimu bora kwa Wanafunzi. Baadhi ya

www.busegadc.go.tz
@busegadc
busegadc
@busegadistrict
halmashauri ya wilaya ya busega

changamoto zilizogunduliwa na Kamati hiyo ni pamoja na kutokuwepo kwa nishati ya umeme katika makazi ya Walimu, uchache wa madarasa, huduma isiyoridhisha ya vyoo na Uhaba wa Nyumba za Watumishi.

Afisa Mipango na Ufuatilia Wilaya ya Busega Bw. Juma Rahisi amesema ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika Shule unafanyika kwa kuzingatia mahitaji ya Shule husika hivyo miundombinu ya Shule hizo itaboreshwa kama ilivyo kwa Shule nyinginezo. Aidha, Bw. Rahisi amewataka viongozi wa Shule kutoa ripoti za mazingira ya Shule mara kwa mara ili kufanyiwa kazi. “Kama kuna mtu ana changamoto yoyote tuwe tunaonana ili kuelezana changamoto”, aliongeza Bw. Rahisi.

Kwa upande wao, Walimu Wakuu wa Shule zote mbili wameshukuru kwa kutembelewa na Kamati hiyo, pia wameomba changamoto ndogondogo zilizopo katika Shule hizo na nyinginezo kufanyiwa kazi ili kuwa na mazingira rafiki katika majukumu yao ya kila siku.

Kamati imefanya ziara katika Shule hizo mbili zilizopo Kata ya Kiloleli ili kuona changamoto zilizopo na kuzifanyiwa kazi. Katika ziara hiyo pamoja na Waheshimiwa madiwani pia Watendaji waliweza kuhudhuria.

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

# Kujifunza Njia ya Kuongeza Mapato ya Halmashauri



**Pichani** ni Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wakiwa katika mnada wa Kidinda uliopo Halmashauri ya Mji Bariadi. Kamati hiyo imefanya ziara katika mnada huo kwaajili ya kujifunza mikakati ya ukusanyaji wa mapato yanayotokana na ushuru wa Mifugo katika mnada huo. Kamati ilipokelewa na Uongozi wa Mnada huo na kujifunza mikakati ambayo itasaidia kuongeza mapato katika Halmashauri ya Wilaya ya Busega.

Awali, Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambae pia ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Mhe. Sundi Muniwe amesema wametembela mnada huo kwa lengo la kujifunza mikakati yenye tija inayotumiwa na Halmashauri ya Mji wa Bariadi katika ushuru utokanao na Mifugo katika Minada ili kuongeza mapato. Halmashauri ya Wilaya ya Busega inaendelea na mikakati ya kuongeza tija katika ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo mbalimbali vya ndani.

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

# Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango Wilayani Busega Yataka Kuimarishwa kwa Usimamizi wa Ukusanyaji Mapato Yatokanayo na Uvuvi



Picha: Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ya Halmashauri ya Wilaya ya Busega ikiongozwa na Mwenyekiti wa kamati hiyo ikiwa imetembelea vyanzo vya mapato vitokanavyo na uvuvi mapema mwezi wa nane mwaka huu.

Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango Wilayani Busega imetembelea vyanzo vya mapato yatokanayo na uvuvi na kutaka mapato ya uvuvi yasimamiwe kwa kina ili kuokoa uwezekano wa upotevu wa mapato ya Halmashauri. Ziara hiyo imefanyika siku ya tarehe 09 Agosti 2021 lengo ni kutembelea na kujionea hali halisi ya mapato yanayotokana na uvuvi Wilayani Busega.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Mhe. Sundi Muniwe anawaagiza maafisa uvuvi Ngazi ya Kata kusimamia vyema

utoaji wa vibali vya kusafirisha samaki kwani wanunuzi wengi wamekuwa sio waaminifu katika ulipaji ushuru

Nae Afisa Uvuvi Wilaya ya Busega Bw. Mwita Mokeha ameeleza kwamba mapato yanayotokana na shughuli za uvuvi yanachangia kwa zaidi ya asilimia 13 katika bajeti ya makusanyo ya ndani ya Halmashauri, lakini bado kuna changamoto katika ukusanyaji ushuru, amewaomba wanunuzi wa samaki kutambua kwamba vibali vyote vya kusafirisha samaki vinatotelewa na maafisa uvuvi waliopo katika Kata husika na sio vinginevyo

Aidha, wajumbe wa kamati hiyo wameomba wadau wa uvuvi wilayani Busega kukaa pamoja na Mwenyekiti wa Halmashauri na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ili kurahisisha suala la ukusanyaji wa mapato, kwani kwa kufanya hivyo itaisadia Halmashauri kukusanya mapato ya kutosha hivyo kusaidia maendeleo wilayani Busega

Nao wavuvi wanasema kwamba hali ya uvuvi kwa sasa imekuwa ngumu kwani samaki wamekuwa wachache ukilinganisha na Miaka ya nyuma na hii inasababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa kwa sasa.

Kamati hiyo iliweza kutembelea mialo ya Ihale, Nyamikoma, Buyolwa na Kashishi, huku Wilaya ya Busega ikiwa na jumla ya mialo 10 inayofanya kazi.

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

# Miradi Saba ya Maendeleo Busega Yatembelewa na Kamati ya Siasa Mkoa wa Simiyu; Kwa Kiasi Kikubwa Yaridhishwa na Utekelezaji Wake



Kamati ya Siasa Mkoa wa Simiyu imeridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo Wilayani Busega katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021. Kamati hiyo imefanya ziara ya siku moja Wilayani Busega siku ya tarehe 16 Agosti 2021.

Katika ziara hiyo wajumbe wa Kamati hiyo wakiongozwa na Mjumbe Halmashauri Kuu Taifa Mkoa wa Simiyu Bw. Emmanuel Silanga imeweza kutembelea Miradi ipatayo 7. Bw. Silanga amesema kwa kiasi kikubwa kamati hiyo imeridhishwa na

Utekelezaji wa Miradi ambayo imetembelewa.

Aidha, Kamati hiyo imetaka ushirikishwaji wa Utekelezaji wa Miradi mbalimbali kwa Wananchi, na Viongozi ikiwemo Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji. Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Simiyu Bw. Mayunga George amesema kumekuwa na malalamiko makubwa kwa Wananchi na Viongozi kuhusu kutoshirikishwa Utekelezaji kwa baadhi ya Miradi.

Kwa upande mwingine Bw. Silanga amesema pamoja na kuridhishwa na kazi nzuri ya Ujenzi wa Miradi ya Maendeleo Wilayani Busega, lakini ni muhimu Miradi hiyo kukamilika kwa wakati ili kuondoa changamoto mbalimbali ambazo ni kero kwa Wananchi. Bw. Silanga ameendelea kwa kusema kwamba Wakanadarasi wengi wamekuwa wakichelewesha Miradi mingi hivyo mamlaka husika zisimamie vyema ili Miradi ikamilike kwa wakati uliopangwa.

Pamoja na hayo, wajumbe wa kamati hiyo wameshauri kwamba ni muhimu taarifa za Fedha za Miradi husika ziwe wazi kwa Wananchi. Aidha, kwa upande mwingine wamemuomba Meneja wa Wakala wa barabara vijijini na mijini (TARURA) Wilaya ya Busega kuwasimamia vyema Wakandarasi wanaoingia nao mikataba ya ujenzi wa Barabara zinazojengwa kuwa na ubora ili ziweze kudumu kwa muda mrefu.

Nae, Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria amesema uongozi wa Wilaya utafanyia kazi maeneo yote yanayoonekana kuwa na changamoto na kuiahidi Kamati hiyo kwamba mapungufu yote yatafanyiwa kazi. Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Busega Bi. Veronica Sayore amesema kwamba ana imani kubwa ya kuendelea kutekeleza Miradi ya Maendeleo na kwamba maelekezo yote yaliyotolewa na Kamati hiyo ili kufikia malengo ya Serikali katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Miradi iliyotembelewa na kamati hiyo ni mradi wa ujenzi wa Zahanati ya imalamate ambayo mpaka sasa umegharimu zaidi ya

www.busegadc.go.tz
@busegadc
@busegadistrict
busegadc
halmashauri ya wilaya ya busega

Tshs Milioni 48, ujenzi kilomita 22 barabara ya Busami-Mwanangi na Bombabija-Kajila Katekista kwa thamani ya zaidi Tshs Milioni 100, mradi wa ujenzi wa wodi 3 Hospitali ya Wilaya; Wodi ya Wanaume, Wanawake na Watoto kwa thamani ya Tshs Milioni 500, mradi wa miundombinu ya Madarasa na Maabara katika Shule mpya ya Sekondari Venance Mabeyo ambapo mpaka sasa thamani iliyotumika ni zaidi ya Tshs Milioni 92, ujenzi wa Madarasa Shule ya Msingi Mwabasabi kwa thamani zaidi ya ya Tshs Milioni 72.8, na mradi wa ujenzi wa tanki la maji Kata ya Mkula kwa thamani ya Tshs Bilioni 2.1.

## TARURA Yatakiwa Kuwasimamia vyema Wakandarasi wa Barabara



Picha: Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria (kushoto) akiwa na wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama Wilaya ya Busega akipata maelezo kutoka kwa Kaimu Meneja TARURA Wilaya ya Busega Mhandisi Pascal Masali (wa kwanza kulia).

Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Busega ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria imeitaka Ofisi ya Wakala wa

www.busegadc.go.tz
@busegadc
@busegadistrict
busegadc
halmashauri ya wilaya ya busega

Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) Wilaya ya

Busega kuwasimamia vyema Wakandarasi wanaojenga barabara Wilayani Busega ili kuharakisha ukamilikaji wa barabara kwa wakati. Maagizo hayo yametolewa siku ya tarehe 29 Julai 2021 wakati kamati hiyo ilipofanya ziara ya kukagua miradi ya barabara kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021.

Kamati hiyo imetembelea barabara takribani 11 zilizopo kwenye mpango wa ujenzi na ukarabati kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kwa kiasi kikubwa kamati hiyo imeridhihswa na ukamilikaji wa barabara hizo lakini imeigiaza Ofisi ya TARURA kuhakikisha ujenzi wa barabara hizo unakamilika ndani ya mikataba iliyowekwa. Kwa upande mwingine kamati hiyo imeridhishwa na barabara zilizotengenezwa kwa kiwango cha Moram, kwani barabara zimeonekana kuimarika na kudumu kwa muda mrefu.

Mhe. Gabriel Zakaria amemuagiza Kaimu Meneja TARURA Wilaya ya Busega Mhandisi Pascal Masali kwamba Wakandarasi wote wanaojenga barabara zilizopo Wilaya ya Busega kufika Ofisini kwake kwaajili ya mazungumzo.

Kwa upande wake Kaimu Meneja TARURA Wilaya ya Busega Mhandisi Paschal Masali amesema baadhi ya wakandarasi wamekuwa wakifanya kazi kwa kasi ndogo na hii inasababishwa na kutokuwa mitambo ya kutosha. Mhandisi Masalia, amesema barabara nyingi zilizopo kwenye matengenezo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 zimekamilika lakini chache miongoni mwa hizo ujenzi wake unaendelea.

Pamoja na mambo mengineyo, Mhe. Gabriel Zakaria amewataka wananchi wa Wilaya ya Busega kutumia vyema miundombinu ya barabara ili ziweze kutumika kwa muda mrefu. Katika ziara hiyo kamati ya Ulinzi na Usalama imeweza kushuhudia uharibifu wa miundombinu ya barabara, kwani wananchi katika baadhi ya maeneo wamekuwa wakitupa taka katika hifadhi za barabara.

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

TARURA Wilaya ya Busega imeweza kujenga na kukarabati barabara zenye urefu wa jumla ya kilomita 98.89 kwa gharama ya TZS Milioni 621.7 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na mpaka sasa Wakandarasi wamelipwa TZS Milioni 327. Huku mwaka wa fedha 2021/2022 TARURA inatarajia kujenga na kukarabati barabara zipatazo 18 kwa thamani ya zaidi ya TZS Bilioni 2.2, kati ya barabara hizo, 6 ni mpya ambazo zitagharimu TZS Bilioni 1 na zitajengwa kwa kiwango cha Moram kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha.

# RC Kafulila: Ni Jukumu la Viongozi Kukutana na Wananchi na Kusikiliza Kero Zao



Picha: Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. David Kafulila akiongea na kujibu hoja za kijiji cha Mwamkara kilichopo Kata ya Nyaruhande Wilayani Busega.

Mkuu wa mkoa wa Simiyu Mhe. David Kafulila amesema ni jambo la msingi viongozi kukutana na Wananchi ili kusikiliza kero na changamoto zinazowakabili.

Ameyasema hayo wakati wa mkutano wa hadhara na Wananchi wa kijiji cha Mwamkara,

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

kilichopo Kata ya Nyaruhande Wilayani Busega siku ya tarehe 13/07/2021.

“Ni wajibu wangu kuhakikisha ninawafikia wananchi na kuzungumza nao, kwakuwa Serikali yetu ni sikivu”, amesema Mhe. Kafulila. Amewataka wananchi wa kijiji cha Mwamkara kuwaamini viongozi waliopo katika ngazi zote na wasisite kuwasilisha kero zao kwa Viongozi hao.

Mhe. Kafulila amesikiliza kero za wananchi katika kijiji hicho, ambapo wananchi wameweza kuwasilisha kero zao, zikiwemo uhaba wa maji safi na salama, ukosefu wa miundombinu ya barabara, mgogoro wa ardhi, huduma za afya na uhaba wa watumishi wa kada ya elimu. Mhe. Kafulila amesema amezipokea kero zote na yupo tayari kuwasiliana na mamlaka zinazohusika ili zifanyiwe kazi na zile zinazotakiwa kutatuliwa kwa muda mfupi zitafanyiwa kazi.

Akijibu kero ya ukosefu wa Zahanati katika kijiji hicho Mkurugenzi Mtandaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega, Bw. Anderson Kabuko, amesema tayari upo mpango wa kujenga kituo cha Afya huku kiasi cha Tshs Milioni 200 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 zimetengwa kwaajili ya kuanza ujenzi wa kituo hicho. Aidha, Kabuko amesema Wilaya ipo katika mpango wa ujenzi wa Shule 24 za Sekondari ifikapo 2025, hivyo kupitia mpango huo utasaidia kupunguza kero ya msongamano wa Wanafunzi katika shule za Sekondari.

Kwa upande mwingine Mhe. Kafulila amesisitiza kutolewaji wa taarifa za fedha zinazojumuisha mapato na matumizi kwa wananchi ili waweze kufahamu matumizi ya fedha katika miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa. “Taarifa za fedha ziwekwe kwenya mbao za matangazo ili wananchi wajue matumizi ya fedha hizo ikiwemo zile zinazoletwa na Serikali na zile zinazotokana na michnago ya wananchi”, aliongeza Kafulila.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria amesema wananchi wa kijiji cha Mwamkara wanastahili kujipongeza kwa kutembelewa na uongozi wa Mkoa na ameahidi kushirikiana na kijiji hicho ili kutekeleza azma ya Serikali ya kuwatumikia wananchi. Mhe. Zakaria amesema kikao hicho ni muhimu kwani licha ya kuwa na majukumu waliyonayo viongozi lakini wameweza kufika katika kijiji hicho na kukutana na wananchi ili wasikilize changamoto na kero zao.

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

# Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira Yatembelea Viwanda vya Kuchambua Pamba na Uzalishaji wa Mafuta

Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira Halmashauri ya Wilaya ya Busega imetembelea Viwanda vidogo vya Uzalishaji wa mafuta ya kupikia na uchambuaji wa Pamba. Ziara hiyo imefanyika siku ya tarehe 02 Agosti 2021 ikiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Charles Lukale.

Wajumbe wa kamati hiyo walifika katika kiwanda cha uzalishaji mafuta kijulikanacho kama LAMADI OIL na kujionea njia zinazotumika kuzalisha mafuta ya kupipikia yanayotokana na zao la Pamba. Mwenyekiti wa kamati hiyo Mhe. Charles Lukale amesema kamati hiyo imetembelea Viwanda hivyo ikiwa ni sehemu ya kujifunza ili kupata ujuzi ambao unaweza kuisaidia Halmashauri kuwekeza katika Viwanda.



Pichani ni Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira ikiwa katika Kiwanda cha kuzalisha mafuta kijulikanacho kama LAMADI OIL na kujionea njia zinazotumika kuzalisha mafuta ya kupipikia yanayotokana na zao la Pamba.

Mkurugenzi wa Kiwanda LAMADI OIL, Bw. Makubi Joseph amesema licha ya kiwanda hicho kuzalisha lita takribani 1,890 kwa siku bado kuna uhaba wa upatikanaji wa Pamba ya kutosha ili kufanya uzalishaji kuwa mkubwa zaidi. Aidha, Bw. Joseph amesema uzalishaji mdogo pia unachangiwa kwa kutokuwa na mtaji wa kutosha, kwani imekuwa ni changamoto kubwa wanapoenda kuomba mikopo katika baadhi ya taasisi za fedha.


www.busegadc.go.tz
@busegadc
@busegadistrict
busegadc
halmashauri ya wilaya ya busega

Kamati hiyo pia imetembelea kiwanda cha kuchambua Pamba na kukamua Mafuta kijulikanacho kama CHESANO COTTON LIMITED na kuridhishwa na hali ya Uzalishaji wake ambapo kwa siku kina uwezo wa kuzalisha Pamba nyuzi zaidi ya tani 26,000. Mkurugenzi wa kiwanda hicho Bw. Peter Bahinya anasema uzalishaji wa kiwanda unategemea zaidi upatikanaji wa Pamba, lakini ana imani kubwa kwamba msimu wa uzalishaji wa Pamba ujao kutakuwa na upatikanaji mkubwa wa Pamba.

Kwa kiasi kikubwa wajumbe wa kamati hiyo wameridhishwa na Uzalishaji wa Mafuta na uchambuaji wa Pamba, ambao unafanyika Wilayani Busega, kwani kupitia Viwanda hivyo kumekuwa na fursa kwa wananchi wa Busega, lakini imewataka wawekezaji wengine kuja kuwekeza Busega. Aidha, wameitaka Ofisi ya Mkurugrnzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega kufuatilia kwa ukaribu kodi itokanayo kna Viwanda hivyo na vingine ili kuongeza ukusanyaji wa mapato.

## Kafulila Awatoa Hofu Wananchi wa Kiloleli Dhidi ya Changamoto Zinazowakabili

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. David Kafulila amefanya ziara Kata ya Kiloleli Wilayani Busega kwaajili ya kusikiliza kero za wananchi wa Kata hiyo siku ya tarehe 24 Septemba 2021, na kuwatoa hofu juu ya kero na changamoto zinazowakabili.




Picha: Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. Gabriel Zakaria akiongea katika mkutano wa hadhara katika Kata ya Kiloleli, Wilayani Busega.

Mkutano huo uliochukua takribani masaa matatu umewapa fursa wananchi wa Kata ya Kiloleli kueleza kero na changamoto zinazowakabili. Miongoni mwa

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

kero zilizowasilishwa na wananchi hao ni pamoja na changamoto za upatikanaji wa maji baadhi ya maeneo, changamoto ya barabara, umeme, maji na uvamizi wa wanyama wakiwemo Viboko na Tembo.



**Picha: Mkazi wa Kata ya Kiloleli akiongea katika mkutano wa hadhara, ambapo Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. David Kafulila alifika katika Kata hiyo kusikiliza kero za wananchi mwishoni mwa mwezi Septemba 2021.**

Pamoja na wananchi hao kueleza kero zao mbele ya Mhe. Kafulila ambapo aliwataka wataalam alioambatana nao kutoka Wilayani Busega kutoa maelezo ya changamoto zilizowasilishwa na wananchi na zile ambazo hazikuwa na maelezo ya papo hapo aliwaeleza wananchi wa Kata hiyo kwamba ataendelea kuzifuatilia kwaajili ya kuzipatia utatuzi.

Mbali na hayo, Mhe. Kafulila amewatoa hofu wananchi wa Kiloleli kwa kuwaeleza kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ina azma na malengo ya kuhakikisha inasimamia Utekelezaji wa Miradi mbalimbali ili kutekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Aidha, Mhe. Kafulila amesema kwamba kwa kudhiirisha hilo, tayari Serikali ya Awamu ya Sita imeweza kuleta fedha kwaajili ya Miradi mbalimbali ikiwemo Miradi ya Elimu, Afya, Maji na Barabara. “Mkoa wetu umepokea kiasi cha Tshs Bilioni 12 kwaajili ya ujenzi

wa Barabara Vijijini, zaidi ya Tshs Bilioni 8.8 kwaajili ya Miradi ya Maji, na miardi mingine mingi", aliongeza Kafulila.

Wananchi wa Kata hiyo pamoja na kueleza kero na changamoto zao pia wameiomba Serikali kujenga chuo cha ufundi Mkoa wa Simiyu na Wilayani Busega ili kuwawezesha vijana ambao hawapati nafasi ya kuendelea na elimu ya sekondari na elimu ya juu kujinga na masomo ya ufundi. Akieleza kwa kina juu ya suala hilo Mhe. Kafulila amesema katika Mkoa wa Simiyu hakuna vyuo vya ufundi ambavyo vipo chini ya VETA, lakini juhudi tayari zimeanza hivyo taratibu zote zikikamilika Mkoa utapata chuo cha ufundi VETA ili kuwawezesha vijana kupata fursa ya masomo ya ufundi, hivyo wananchi wawe na subira.

Mhe. Kafulila anaendelea na Utaratibu wake wa kusikiliza kero za wananchi maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Simiyu, na hii ni zaidi ya mara tatu kufanya ziara ya kusikiliza kero za wananchi Wilayani Busega.

## Wanaojihusisha na Uhalifu Busega Waonywa

Mkuu wa Wilaya ya Busega ambae pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Busega, amesema hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wote wanaojihusisha na uhalifu, ambapo siku za hivi karibuni kumekuwa na malalamiko ya uhalifu ikiwemo wizi katika maeneo mbalimbali Wilayani Busega. Mhe. Zakaria ameyasema hayo wakati alipofanya mkutano



**Picha: Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria akiongea na wananchi wa Kata ya Nyashimo ambapo ndipo makao makuu ya Wilaya ya Busega. Mhe. Zakaria alifanya ziara ya kusikiliza kero na changamoto ya wakazi wa Kata hiyo.**

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

wa hadhara kusikiliza kero za wananchi wa Kata ya Nyashimo, tarehe 22 Septemba 2021.

Wakitoa kero zao wakazi wa Kata hiyo wanasema kwamba, hali ya uhalifu imekuwa ikiongezeka na kueleza kwamba hali hiyo imekuwa ikileta taharuki kubwa kwa wakazi wa Kata hiyo na Wilaya kwa ujumla. Wanaeleza kwamba kumekuwa na vikundi vinavyojihusisha na wizi wa kupora na kuvunja nyumba na kuiba mali mbalimbali ikiwemo fedha na vitu vingenevyo.

“Ni kweli nimepata malalamiko za uhalifu hasa wa uporaji, lakini nataka kusema watu wasijaribu kufanya uhalifu, mimi na vyombo vyangu vya ulinzi tupo macho na tunaendelea kuwabaini wote ambao wanajihusisha na uhalifu, ili hatua zaidi zichukuliwe dhidi yao”, aliongeza Mhe. Zakaria.

Wananchi wa Kata hiyo wameomba Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kuchuku hatua za haraka ili kuhakikisha uhalifu ambao umeanza kushamiri maeneo mablimbali Wilayani Busega unakomeshwa kwa kuwashughulikia wote wanaojihusisha na matukio hayo.

Pamoja na mambo mengineyo, wananchi wa Kata ya Nyashimo wameweza kueleza kero mbalimbali ikiwemo changamoto ya mioundombinu ya barabara za vijiji, uwepo wa soko la Wilaya, na eneo la makaburi ya Wilaya, huku ufafanuzi wa kina ukitolewa juu ya kero hizo. Mhe. Gabriel Zakaria anaendelea kusikiliza kero za wananchi maeneo mbalimbali za Wilaya ya Busega, ikiwa ni utaratibu aliojiwekea.